

Fahamu Haki Zako: Usaidizi Kwa Wanafunzi Wasio Na Makao



Je,

- Unaishi na marafiki au jamaa wa ukoo?
- Unaishi kwenye hoteli au moteli?
- Unaishi kwenye kimbilio?
- Unaishi kwenye gari au RV?
- Unaishi pahali popote ambapo si makao ya kudumu?

Mtoto wako ana haki!

Mtoto wako ana haki ya:

- **KUSALIA** katika shule aliyomo sasa hivi AU
- **KUJIANDIKISHA KWA MASOMO** katika wilaya ya shule unakoishi.
- **KUANZA** mafunzo na **KUHUDHURIA** shughuli za shule mara moja huku hati za kujiandikisha zikiendelea kukusanywa.
- **KUPATA USAIDIZI WA ZIADA** bila malipoili kufanya vyema shuleni.

Je, unahitaji usaidizi?

- **PIGA SIMU** kwa wilaya ya shule. **OMBA** kuzungumza na afisa ushirikiano wa McKinney-Vento. **Una haki ya kupata kesi yako kusikizwa.**
- **PIGA SIMU** kwa Idara ya Elimu ya Ohio kupitia nambari: 614-387-7725 au 877-644-6338. **OMBA** kuzungumza na Mratibu wa McKinney-Vento.
- **TUMA** barua kwa shule ukiomba usaidizi. **HIFADHI** nakala. (Picha ya barua yako uliyohifadhi kwenye simu itafaa vyema.)

Je, unaweza kupata usaidizi wa aina gani?

- Usaidizi wa kukuwezesha kusalia katika shule ambayo unasomea kwa sasa
- Usaidizi wa kujiandikisha katika shule mpya
- Usafiri
- Milo ya shule bila malipo
- Sare za shule
- Bidhaa zinazotumika shuleni
- Shughuli na huduma za baada ya shule zinazotolewa na shule
- Misamaha ya karo ya shule
- Kupata nakala za taarifa za chanjo
- Kupata nakala za vyeti vya kuzaliwa
- Rufaa kwa huduma za afya, ushauri nasaha, matibabu ya meno na huduma zinginezo

Ikiwa Unahitaji Usaidizi wa Kisheria Bila Malipo:



PIGA SIMU:

Legal Aid Line of Western Ohio:
SIMU ISIYO NA MALIPO:
(888) 534-1432

TUMA OMBI MTANDAONI:

Wavuti ya Legal Aid Line:
www.legalaidline.org



Advocates for Basic Legal Equality, Inc. na Legal Aid of Western Ohio, Inc. (ABLE) ni mashirika ya kisheria yasiyo ya faida yanayoshughulikia mahitaji ya kisheria ya kiraia ya watu binafsi na familia zilizo na mapato madogo katika magharibi mwa Ohio. Habari hizi si ushauri wa kisheria. Ni habari za kawaida. Habari hizi hazitumiki kama mbadala wa kuzungumza na wakili kuhusu hali yako. Huenda bado ukahitaji usaidizi kutoka kwa wakili.

*Ilisashwa kwa mara ya mwisho Novemba 19, 2019

Mradi huu ulifadhiliwa kwa ruzuku kutoka kwa Shirika la Dayton Legal Heritage Foundation la Dayton Foundation.

